# KANUNI ZA KIFEMINISTI ZA MATUMIZI YA MTANDAO



INITIATIVE FOR EQUALITY AND NON DISCRIMINATION (INEND)

INEND
INITIATIVE FOR EQUALITY AND NON DISCRIMINATION
"Dignified Lives"

**UCHAPISHAJI**

**Kanuni hizi zimechapishwa na shirika la kutetea haki za kibinadamu la Initiative for Equality and Non Discrimination (INEND), Oktoba 2020.**

**Kanuni hizi zimeungwa mkono na Shirika la Association for Progressive Communication, (APC).**

**WAHUSIKA**

Mtafsiri: Helen Mudora
Wahariri: Wanafeministi katika miji ya Mombasa, Kisumu na Nairobi
Mpangilio wa Muundo: Arafa Hamadi
Uchoraji: Arafa Hamadi

**MATUMIZI**

Uko huru kugawa, kunakili/kupiga chapa na kusambaza tena kanuni hizi kwa mbinu au aina yoyote ile kwa masharti yafuatayo:- Sharti utoe sifa na uonyeshe iwapo mabadiliko yoyote yamefanyika. Uko na uhuru wa kufanya hivyo ila si kwa njia itakayoonyesha kwamba mchapishaji wa kanuni hizi ameidhinisha hatua hiyo.

Matumizi yasiyo ya kibiashara: hauna uhuru wa kutumia kanuni hizi kwa biashara yoyote.

**KUTUHUSU**

Initiative for Equality and Non Discrimination (INEND) ni shirika la kutetea haki za binadamu katika mkoa wa Pwani, lililoundwa katika mwaka wa 2015. INEND hufanya utafiti na kuchukua hatua na mikakati ambayo inapelekea usawa, kukubalika na kujumuishwa kwa kila mwanadamu katika jamii. Tunashirikiana na mashirika na washikadau wengine ili kuhakikisha kutobaguliwa kwa watu walio na maumbiletofauti ya kijinsia na kimpanzi na wengine.

# Utangulizi

Kanuni zifuatazo ni muhimu ili kuinua kigezo cha mtandao ambao unazingatia usawa wa kijinsia na wa watu wote. Mtandao wa kifeministi huanza na kuwezesha wanawake, na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia kufurahia mtandao ambao ni wa kukubalika, kujimudu, uwazi, maana, usio na masharti, na unaopatikana kwa urahisi na kwa usawa.

Mtandao wa kifeministi huwezesha wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia kufurahia tofauti zetu, haki zetu, huku tukivunja misingi ya mfumo dume. Hali hii inajumuisha tofauti za hali zetu, na muktadha, kama vile tofauti za umri, jinsia, ulemavu, tabaka mbali mbali, hali zetu za kiuchumi, imani na misimamo tofauti za kisiasa na kidini, kikabila na rangi za ngozi zinazotutenganisha. Kanuni zifuatazo ni muhimu katika kuafikia malengo ya mtandao wa kifeministi;-.

# 1 Ufikiaji sawa wa mtandao

Mtandao wa kifeministi huanza na kuwezesha wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia kufurahia huduma za mtandao kwa bei nafuu, bila masharti zinazokubalika, zilizo wazi, na ufikiaji sawa ulimwenguni.



# 2 Kupata/Ufikiaji Habari


Tunakubaliana na kulinda haki ya kupata habari muhimu kwa wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia. Habari hii inahusu haswa haki na afya za kingono na uzazi , raha, njia salama za uavyaji mimba, ufikiaji wa haki na maswala ya Muungano wa LGBTQGNC++

Habari hizi zitazingatia tofauti katika lugha, muktadha, uwezo na mapendeleo za kibinafsi.



# 3 Matumizi ya teknolojia

Wanawake, watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia wana haki ya kutengeneza msimbo (code), kubuni,kubadilisha na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) kwa njia endelevu. Wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia pia wana nafasi ya kutawala katika sekta ya teknolojia kama jukwaa la ubunifu na kujieleza, vile vile na kupambana na changamoto za kitamaduni za ubaguzi wa kijinsia na ubaguzi kwa ujumla.



# 4 Dhana Mbadala

Mtandao ni mahali ambapo kanuni za kijamii hujadiliwa na kuzingatiwa, hali ambayo inatokana na itikadi za kueneza mfumo dume, na kuchangia chuki kwa watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia. Tunasisitiza mtandao wa kifeministi ambao unahusisha dhana tofauti kwa hali na sehemu zote, iwe ni hadharani au sehemu za kibinafsi.



# 5 Uanaharakati

Tunaelewa kwamba mtandao ni mahali panapoweza kubadili mawazo ya watu. Kwa hivyo, mtandao una uwezo wa kujenga uraia upya ambao unawezesha watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia kujitambua na kujieleza. Zaidi ya hayo, mtandao una uwezo wa kuunganisha watu wa jinsia tofauti ulimwengu mzima, ukisisitiza uwazi na uwajibikaji pamoja na kutengeneza muungano endelevu wa kifeministi.



# 6 Kufanya Maamuzi katika utawala wa mtandao

Tunaamini ya kwamba mifumo kama mfumo dume ambao umechangia kwa ukubwa mawazo na mwongozo wa mtandao waweza kubadilishwa, hasa tukisisitiza kujumishwa kwa wale wanaopigania usawa wa kijinsia na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia katika uongozi wa mtandao. Tungependa demokrasia izingatiwe katika kuunda sera ambazo zinaaathiri umiliki na utumizi wa mtandao duniani kote.



# 7 Uchumi Mbadala

Tunazingatia kuchunguza fikra za kibepari zinazoendeleza teknolojia kwa kusisitiza ubinafsishaji, na kujifaidisha. Tunajitolea kuunda njia mbadala za utawala wa kiuchumi zilizo na msingi kwenye kanuni za ushirikiano, umoja, ujamaa, uhifadhi wa mazingira na uwazi.





# 8 Mtandao wazi usio na malipo

Tunania ya kubuni na kufanya majaribio na teknolojia, tukizingatia usalama wa kidijitali na matumizi ya programu (software) za bure kama vile FLOSS. Tunasisitiza kukuza , kusambaza, kuelimisha na kueneza maarifa ya teknolojia ya FLOSS .

# 9 Kukuza mazungumuzo ya Kifeministi

Tunadai ubingwa wa mtandao kukuza habari za matukio halisi ya wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia. Tunapinga na kukataa kudhalilishwa kwa sauti za wafeministi na wanaharakati wa haki za kibinadamu na nguvu za kiserikali, dini na vikundi vilivyo na misimamo mikali ambayo inaamua na kutawala maadili.



# 10 Uhuru wa kujieleza


Tunatetea haki na umuhimu wa usemi wa hisia za kimapenzi kama swala la uhuru wa kujieleza na lisilo duni ya semi zingine kama vile za kidini na kisiasa. Tunapinga vikali juhudi za serikali na mashirika kudhibiti, kuchunguza, na kuzuia semi za kifeministi, watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia kwenye mtandao, matumizi ya teknolojia, na sheria.

Tunatambua hii kama njama kudhibiti maadili na ujenzi wa vigezo vya uraia na haki za kibinadamu.



# 11 Pornografia na maudhui ya madhara

Tunatambua kuwa swala la pornografia kwenye mtandao linahusiana na wakala, idhini na uwezo. Tunapinga kusawasisha na kujumishwa kwa pornografia na unyanyasaji dhidi ya wanawake au kulinganishwa na maudhui yenye madhara ili kudunisha kujieleza kwa wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia. Tunaunga mkono juhudi za kujieleza kwa kubuni maudhui mbadala na utawala wa mfumo dume ambao hudhibiti na kudhalilisha wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia.



# 12 Idhini

Tunatoa mwito wa kutungwa kwa maadili na siasa za idhini katika tamaduni, muundo, sera na masharti ya utumiaji wa majukwaa ya mitandao. Tunaamini kwamba kujieleza kwa wanawake inategemea uwezo wao wa kufanya maamuzi kuhusu mambo yao ya siri au mambo ya umma watakao sambaza kwenye mtandao.



# 13 Faragha na data

Tunaunga mkono haki ya kila mtu kuwa na faragha na udhibiti wa habari za kibinafsi katika viwango vyote vya mtandao. Tunapinga hatua ya serikali na mashirika ya kibinafsi kutumia data kwa ajili ya kupata faida na kutoa habari za kupotosha kuhusu tabia na mapendeleo ya kibinafsi Tunatambua uchunguzi kama chombo cha kihistoria cha mfumo dume unaotumiwa kudhibiti miili, maongezi na uwanaharakati wa wanawake. Pia tunaangazia tabia za udhibiti unaotokana na matendo ya watu binafsi, mashirika ya kibinafsi na washika dau wasio wa kiserikali.



# 14 Kumbukumbu

Tunahaki ya kuwa na umiliki juu ya historia na kumbukumbu zetu katika mtandao. Hii inajumuisha kuweza kupata data na habari zinazotuhusu mtandaoni, na kuweza kudhibiti pamoja na kujua nani ana uwezo wa kufikia habari zetu za kibinafsi na kuwa na uwezo wa kuzifuta hizi data milele.



# 15 Kutojulikana

Tunatetea haki ya kutojulikana na kukataa madai yote ya kuzuia kutojulikana kwenye mtandao. Kutojulikana kunawezesha uhuru wetu wa kujieleza kwa mtandao, haswa maswala ya kuvunja miiko ya ujinsia na itkadi za ubaguzi, kufanya majaribu ya kujitambulisha kijinsia, na kuwezesha usalama kwa wanawake na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia katika jamii ulioathiriwa na ubaguzi.



# 16 Watoto na vijana

Tunatoa mwito wa kushirikishwa kwa vijana kwa maamuzi ya usalama wao wakiwa kwenye mtandao, faragha , ukuzaji wa usalama wao, na upatikanaji wa habari. Tunatambua haki ya watoto kwa afya, kihemko, kupata habari sawa kuhusu ngono na jinsia, kwa wakati unaofaa.



# 17 Vita vya kimtandao



Tunatoa wito kwa wadau wote wa mtandao pamoja na watumiaji wa mtandao, watunga sera, na sekta za kibinafsi kushughulikia swala la unyanyasaji na vita katika mtandao na za kiteknolojia. Tunaelewa ya kwamba kuna visa vingi vya mashambulizi na vitisho dhidi ya wanawake, na watu wenye hisia tofauti za kimapenzi na jinsia. Hali hii ni ya kushangaza, na ina madhara kwa wanaolengwa na hivi vitisho na mashambulizi. Ni jukumu letu wote kuimarisha uwajibikaji wetu dhidi ya swala nzima la unyanyasaji wa kijinsia.

# KANUNI ZA KIFEMINISTI ZA MATUMIZI YA MTANDAO

INEND
INITIATIVE FOR EQUALITY AND NON DISCRIMINATION
"Dignified Lives"

www.inend.org
info@inend.org
P.O BOX 10315-80101
Mombasa, Kenya

@INENDorg @inend.ke
Initiative for Equality and Non Discrimination